

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA NANE

01 JUNI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA NANE – TAREHE 01 JUNI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

491. MHESHIMIWA ERIC JAMES SHIGONGO (BUCHOSA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Vifaa Tiba vya Hospitali ya Wilaya ya Buchosa vitanunuliwa.

492. MHESHIMIWA STANSLAUS SHING'OMA MABULA (NYAMAGANA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni kutoa fedha za ujenzi wa Vituo vya Afya kwa kigezo cha idadi ya Tarafa ni kuwanyima Wananchi Vituo vya Afya.

493. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Ihanu - Mufindi.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

494. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali imefikia wapi katika mpango wake wa kurudisha Reli ya Mtwara – Mbamba Bay na eneo la Mchuchuma.

495. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaweka taa za kuongoza magari Igunga Mjini kwenye makutano ya Barabara kuu ya Singida – Mwanza ili kuepusha ajali.

496. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA (KILINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga Daraja linalounganisha Kata ya Bokwa na Songe Kilindi.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

497. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mpango gani wa kubadilisha utaratibu wa utoaji vibali vya kuvuna miti ili kuhusisha Kamati za Maendeleo za Kata na Vijiji.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

498. MHESHIMIWA AMOUR KHAMIS MBAROUK (TUMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kwanini Serikali imehamisha Kituo Kidogo cha Polisi Tumbwe.

WIZARA YA AFYA:

499. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama za matibabu kwa Akinamama wanapokwenda Kliniki Sumbawanga.

WIZARA YA KILIMO:

500. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itakarabati Skimu za Umwagiliaji za Katengera, Ruhwiti na Muhwazi ili kuboresha kilimo cha umwagiliaji Kakonko.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NISHATI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
01 JUNI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**